

**TAASISI YA NCHI ZA ASIA NA AFRIKA, CHUO KIKUU CHA
MOSCOW**

UCHUNGUZI WA KISWAHILI KATIKA URUSI*

NELLY V. GROMOVA

Utafiti wa lugha ya Kiswahili katika Urusi ulianza mwishoni mwa karne ya 18 Wakati ule kwa mara ya kwanza katika historia ya sayansi ya Kirusi ilianza kutolewa "Kamusi ya ulinganisho wa lugha zote za dunia" mnamo mwaka 1791 Akademia ya sayansi ya Urusi ilikusanya katika Kamusi hiyo maneno kadhaa ya lugha 33 za dunia, miongoni mwao zikiwemo lugha 6 za Kibantu.

Jaribio jingine la kukusanya data zilizopo za lugha za Kiafrika lilikuwa ni uchapishaji wa kitabu kijulikanacho kwa jina la *Mitridates oder allgemeine Sprachkunde*. Kitabu hicho kilikuwa na juzuu 4, zilizotolewa kuanzia mwaka 1806 hadi 1817. Na katika nyongeza ya juzuu ya 4 tu iliyotungwa na Friederich Adelung yamepatikana maneno ya Kiswahili. Maneno hayo yalikuwa yameandikwa na msafiri wa Kiingereza bw. Henry Salt aliyetembelea Afrika Mashariki mnamo miaka 1809-1810. Kati ya maneno hayo yamo majina ya udugu (kama yale: mama, baba, mwana, ndugu, mke, n k), majina ya hesabu kuanzia moja hadi kumi na maneno mengine kama maji, moto, nyumba, mlima na mengineyo.

Wachunguzi karibu wote walioshughulika na lugha za Kibantu wanadai kwamba hiyo ndiyo kamusi ya kwanza ya lugha ya Kiswahili Lakini katika idara ya maandiko ya maktaba ya Petersburg inahifadhiwa kamusi ndogo iliyotungwa na kapteni Thomas Smee mnamo mwaka 1811 Kamusi hiyo ina maneno yapatayo 100 hivi (Olderogge 1971).

Hivyo basi inawezekana kusema kwamba mwanzoni mwa karne ya 19 warusi walikuwa na uwezekano wa kujijulisha na lugha ya Kiswahili. Lakini utafiti hasa wa lugha za Kiafrika katika Urusi ulihusu ukoo wa Kisemetiki tu. Mwanzoni mwa karne ya 19 lugha kogwe ya Kihabeshi ilianza kufundishwa kwenye Chuo Kikuu cha Kharkov (mwaka 1829, prof Dorn), Chuo Kikuu cha Kiyev (mwaka 1861, prof Uspenskiy) na baadaye katika Chuo kikuu cha Petersburg (mwaka 1896, prof. Turayev) Wataalamu warusi walichunguza pia lugha kongwe ya Kimisri Sayansi ya Kirusi ilijipatia mafaniko mema katika fani hizo.

* Makala haya yalitolewa katika 7 Swahili Colloquium, Bayreuth, 13/14 May 1994

Lakini uchunguzi kamili wa lugha za Kiafrika hasa lugha hai ulianza katika Urusi baada ya Mapinduzi ya Oktoba yatokee. Na lugha ya kwanza ya Afrika ya kitropiki iliyofundishwa katika Urusi ya kisoviet ilikuwa ni lugha ya Kiswahili. Mnamo mwaka wa 1929 huko Leningrad lilikuwa likianzishwa kundi la kuchunguza mambo ya kisiasa ya Afrika na Dmitry Olderogge alianza kuwafundisha wanakozi hao lugha ya Kiswahili (baadaye akawa profesa wa Chuo Kikuu cha Leningrad na memba mwandishi wa Akademia ya sayansi ya Urusi). Hivyo basi, historia ya kujifunza na kutafiti kwa Kiswahili katika Urusi inahesabu zaidi ya nusu karne.

Uteuzi wa lugha ya Kiswahili iwe lugha ya mafunzo ulitegemea maana na umuhimu wa lugha hii. Kiswahili ilienea sana katika nchi za Afrika Mashariki na kutumiwa na makabila mengi tangu zamani. Kadiri ya wazungumzaji wa Kiswahili inazidi milioni 50 hivi.

Uchunguzi wa kinadharia wa Kiswahili ulianza kuendelezwa katika Urusi ya kisoviet mnamo miaka ya 30. Mnamo miaka hiyo hapo Moscow ilikuwa imeundwa Taasisi maalum zilizoshughulika na mambo ya Afrika na kati yao ilikuwa ni Tume ya lugha iliyoko chini ya Shirika la uchunguzi wa kisayansi wa maswali ya kitaifa na ya kikoloni. Mkuu wa Tume hiyo alikuwa prof. G. Danilov, ambaye jina lake limesahaulika kwa muda mrefu. Siku hizi tu ambapo inawezekana kuangalia na kuchunguza hati na karatasi zilizohifadhiwa katika zile maktaba za nyaraka za kichama zisizofunguliwa kwa ajili ya watu wa kawaida, tulipata nafasi ya kujijulisha na kazi za kisayansi zilizofanywa na wataalam wa lugha za Kiafrika walioongozwa na prof. Danilov.

Katika mwaka 1934 hapo Moscow lilifanyika kongamano la kwanza katika Urusi la wanaisimu wa lugha za Kiafrika. Yamejadiliwa maswali mengi yahasuyo hali iliyoko ya lugha za Kiafrika na majukumu ya wanaisimu wasoviet katika uchunguzi wa lugha hizo. Kati ya mada zilizotolewa zilikuwa ni taarifa ya prof. Danilov kuhusu mfumo wa kifonetiki wa kiswahili na taarifa ya bw. P. Kuznetsov juu ya njia za kueleza uhusiano "mtenda-mtendewa" katika Kiswahili (Kuznetsov 1935).

Vile vile kongamano hilo lilithibisha mpango wa kikazi wa uchunguzi wa lugha za Kiafrika. Miongoni mwa kazi hizo zilikuwemo Kamusi za istilahi za kiuchumi na za kijamii za lugha zifuatazo: Kihausa (mtungaji prof. Yushmanov), Kizulu na Kikhosa (mtungaji dr. Snegiryov), Kisutho (prof. Olderoge), Kiswahili (prof. Danilov). Zaidi ya hayo wataalam wasoviet walipanga kutunga sarufi ya lugha ya Kiswahili (mtungaji prof. Olderoge) na ya Kizulu (dr. Snegiryov). Kama ninavyojua, hata kitabu kimoja kati ya vilivyotajwa juu hakikutolewa ama kupigwa chapa mpaka leo. Pengine maandiko ya vitabu hivyo yamo katika maktaba zisizo wazi, sawa na Kamusi ndogo ya Kirusi-Kiswahili, iliyotayarishwa na prof. Danilov mnamo mwaka 1934. Jina lake kamili ni *Kamusi ndogo ya Kirusi-Kiswahili*. Maneno elfu 5 yatumikayo katika lugha ya Kirusi na vitabu vya kisiasa" (Gromova 1994). Kamusi hiyo

ilikuwa na nyongeza mbili, moja ni maelezo ya sarufi ya Kiswahili yaliyoandikwa na dr Kuznetsov, na ya pili ni matini mbalimbali za Kiswahili, hasa ni mazungumzo kati ya watalii, tena makala juu ya chama cha kikomunisti cha Urusi, ubeberu na harakati ya kupinga ukoloni na ukoloni mambo leo, wasifu wa nd. Lenin n k , zilizotafsiriwa katika lugha ya Kiswahili

Kusema kweli, Kamusi hiyo ina makosa mengi ya kisarufi na ya kimsamiati Lakini kamusi hiyo ilikuwa ya kwanza katika Urusi Tena sote tunaoshughulika na utungaji wa kamusi, tunajua kwamba lengo la kuandaa kamusi ya aina hii yaani kamusi ya Kirusi-Kiswahili ama Kijerumani-Kiswahili ni gumu zaidi Katika kazi yake prof Danilov alitegemea kamusi za Krapf (1882), Steere (1882), Büttner (1890), Velten (1910), Binns (1925), Seidel (1928), lakini kamusi hizo zote hazikujaa istilahi za kisiasa Prof G. Danilov alishauriana na wazungumzaji wa Kiswahili waliojifunza wakati ule katika vyuo mbalimbali vya Moscow Jina la mmojawapo linajulikana wazi, huyo ni Jomo Kenyatta, wengine hatujawajua, lakini inaonekana kwamba walikuwa ni Wahindi waliotoka Afrika Mashariki ambao wote walitumia Kiswahili kama lugha ya pili, hivyo baadhi ya makosa ni juu yao

Makala chache zilizohusu vipengele tofauti vya Kiswahili zilikuwa zimetolewa mnamo miaka ya 30 Bw P Kuznetsov (baadaye profesa wa Chuo Kikuu cha Moscow) mwaka 1935 alichapisha makala yenye mawazo muhimu juu ya uainisho wa ngeli za majina na mbinu za upatanisho wa kisarufi wa Kiswahili (Kuznetsov 1935). Alitegemea data zilizopatikana wakati wa kazi yake ya kiutafiti na wazungumzaji wa Kiswahili Maswali ya kutatanisha ya mfumo wa kisarufi wa lugha za Kibantu yaani ngeli za mahali yalizingatiwa na prof D Olderogge katika makala yake iliyotolewa mwaka 1937

Wakati wa Vita Vikuu vya Pili mafunzo na utafiti wa lugha za Kiafrika nchini kwetu ulikuwa umeahirishwa mpaka ulipoanza upya mwaka 1945 kwenye idara ya elimu ya Afrika (uafrikanistika) ya kitivo cha lugha za Mashariki cha Chuo Kikuu cha Leningrad

Siku hizi lugha ya Kiswahili inafundishwa na kuchunguzwa kwenye baadhi ya vyuo vikuu na taasisi za nchi yetu yaani Taasisi ya nchi za Asia na Afrika iliyo chini ya Chuo Kikuu cha Moscow kilichopewa jina la Lomonosov (tangu mwaka 1960), kitivo cha Mashariki cha Chuo Kikuu cha Petersburg (tangu mwaka 1934), Taasisi ya uhusiano wa kimataifa (tangu mwaka 1957), Chuo Kikuu cha urafiki baina ya mataifa kilichoitwa kwa jina la Lumumba (tangu mwaka 1961) Akademia ya kisayansi ya Urusi inajishughulisha vile vile na utafiti wa Kiswahili: katika Taasisi ya elimu ya lugha kuna idara ya lugha za Kiafrika (mkurugenzi wake wa kwanza alikuwa ni prof N. Okhotina, na sasa ni dr A. Vinogradov)

Ndani ya miaka ya 60 uchunguzi wa lugha ya Kiswahili pamoja na lugha nyingine za Kibantu uliendelezwa kwa nguvu zaidi Vilikuwa vimetungwa vitabu kuhusu sarufi ya lugha ya Kiswahili au Kiswahili kikilinganishwa na lugha nyingine za Kibantu, kwa mfano *Lugha ya*

Kiswahili (Miachina 1960), "Aina za maneno katika lugha za kibantu na misingi ya kuzifafanusha" (Gromova 1966) Kuna makala nyingi zihusuzo maswali ya mfumo wa kisarufi wa Kiswahili, mnyambuliko wake, utaratibu wa kifonetiki n.k (watumaji ni I. Aksionova, A. Zhukov, N. Okhotina, N. Potekhina, I. Fedoseeva, N. Fiodorova, I. Yakovleva na wengine) Historia ya Kiswahili na maandishi yake yalichunguliwa na V. Misiugin¹. Na siku hizi wataalam warusi wanafanya utafiti wa Kiswahili wakitegemea misingi mipya kwa kujali mafanikio ya elimu ya lugha yapatikanayo nchini kwetu na katika nchi za nje. Wataalam warusi wanachambua pia maandishi ya fasihi na mashairi ya Kiswahili, matumizi ya lugha n.k. Hivyo inawezekana kusema kwamba wanaelimu warusi wanaochunguza Kiswahili na vipengele vyake tofauti pamoja na nyanja zake zote wanatoa mchango usio mdogo katika nadharia ya elimu ya lugha za Kibantu.

Waalimu wa lugha ya kiswahili nchini kwetu wametunga vitabu vya masomo vinavyohitajika kwa ajili ya kuwafundisha wanafunzi, vitabu vya kiada na vya ziada, vitini n.k. vinavyoweza kufanya mafunzo yawe bora zaidi (Fiodorova 1974, Gromova & Miachina 1975, Gromova & Karpovich 1985). Zimeshatolewa pia kamusi za aina mbili: kamusi za Kiswahili-Kirusi na za Kirusi-Kiswahili kati yao zikiwemo kamusi ya maneno yatumikayo magazetini, Kamusi ya mafunzo na nyinginezo (Olderogge 1961, Kuznetsov 1965, Gromova & Fiodorova 1978) Kamusi ya kwanza ya Kiswahili-Kirusi ilitolewa mwaka 1961 ikiwa na maneno elfu 18 hivi. Ni dhahiri kwamba kamusi hiyo ilihitaji kurekebishwa upya kwa sababu lugha ya Kiswahili inajiendeleza kwa haraka sana na msamiati wake hujazwa na maneno mengi mapya. Hivyo mnamo mwaka 1987 tulichapisha kamusi mpya yenye maneno elfu 30 hivi (Miachina 1987).

Katika kazi yetu ya ualimu sawa na kazi ya utafiti sisi, wataalam warusi wa lugha ya kiswahili, tunakosa mno uhusiano na taasisi za lugha ya Kiswahili zilizoko Tanzania. Kuna mkataba wa utamaduni kati ya nchi zetu mbili, lakini mpaka sasa wataalam wachache tu walipata nafasi ya kutembelea Tanzania ili kufanya bora ujuzi na maarifa yao ya Kiswahili. Tunahitaji vile vile uhusiano wa karibu zaidi na Taasisi na wanaelimu wa nchi za Ulaya wanaoshughulika na fani tofauti za lugha ya Kiswahili. Tungeweza kushirikiana katika uchunguzi wa Kiswahili, kutunga pamoja kamusi, vitabu vya mafunzo, katika kuchapisha kazi za kisayansi za pamoja n.k.

Kwa kumaliza nataka kutilia mkazo kwamba mabadilishano ya maoni huhimiza maendeleo ya fikra za kisayansi, ijapokuwa maoni ya wanaelimu mbali mbali yaweza kutofautiana kuhusu vipengele vya lugha. Lakini tofauti hizo na mgongano wa mawazo unapiga hatua mbele. Naamini kwamba kushirikiana kwetu kitaalam kunawezekana na kutaleta faida kubwa kwa pande zote zihusuzo.

¹ Kuzitaja makala zote za wanaisimu hao kungehitaji kurasa nyingi

Mapitio

- Fiodorova, N G. 1974. *Uchebnik yazika suahili* ("Kitabu cha masomo ya Kiswahili"). Moscow
- Gromova N V. & B B. Karpovich 1985. *Leksikologia na frazeologia yazika suahili*. ("Leksikolojia na nahau za Kiswahili"). Moscow.
- Gromova, N.V 1966. *Chasti rechi v yazikach bantu i printsipi ich razgranicheniya* ("Aina za maneno katika lugha za Kibantu na misingi ya kuzifafanusha") Moscow
- Gromova, N V. 1994. 'Maliy russko-suahili slovar G Danilova', ("Kamusi ndogo ya Kirusi-Kiswahili iliyotungwa na G Danilov"), *Vostok* 3
- Gromova, N V & E N. Miachina 1975. *Uchebnik yazika suahili*. ("Kitabu cha ziada cha Kiswahili") Moscow
- Gromova, N.V, Fiodorova N G. 1978 *Uchebniy russko- suahili slovar* ("Kamusi ya mafunzo ya Kirusi kwa Kiswahili") Moscow
- Kuznetsov, P S. 1935. Ob imennoy klassifikatsii i sisteme soglasovaniya v suahili ("Kuhusu uainisho wa ngeli na mfumo wa upatanisho katika Kiswahili"), in *Yazik zarubejnogo Vostoka* 1/18. Moscow
- Kuznetsov, A I. 1965. *Kratkiy suahili-russkiy i russko-suahili slovar*. ("Kamusi fupi ya Kiswahili-Kirusi na Kirusi-Kiswahili"). Moscow
- Miachina, E. 1987. *Suahili-russkiy slovar*. ("Kamusi ya Kiswahili-Kirusi"). Moscow.
- Miachina, E N. 1960. *Yazik suahili* ("Lugha ya Kiswahili") Moscow
- Olderogge D A. 1937. *Opredeleniye vremeni i prostranstva v yazikach bantu (lokativniye klassi)* ("Ainisho la wakati na mahali katika lugha za Kibantu yaani ngeli za mahali"), in / *Pamyati V.G. Bogoraza* Moscow/Leningrad
- Olderogge, D. 1961. *Suahili-russkiy slovar* ("Kamusi ya Kiswahili-Kirusi") Moscow.
- Olderogge, D A. 1971. 'Slovar yazika suahili 1811', ("Kamusi ya lugha ya Kiswahili ya mwaka 1811"), *Africana, VII*. Leningrad.